

Vitu Saba Unavyohitaji Kujua kabla ya Kufanyiwa Uchunguzi wa Afya

1. Uchunguzi wa afya ni nini?

Uchunguzi wa afya ni uchunguzi wa kina wa afya ya mwili na kihisia ya wanafamilia wote, na unahitajika kama sehemu ya utaratibu wako wa kupata makazi mapya nchini Marekani. Hufanyika katika kliniki maalum na hufanywa na wahudumu wa afya waliohitimu.

2. Nitafikaje huko?

Mtoa huduma wako wa jamii atashirikiana nawe na familia yako ili kupata huduma bora zaidi ya usafiri.

3. Familia yangu ina watoto wenye umri wa kwenda shuleni. Je, ninahitaji kufanya nini katika uchunguzi wangu wa afya?

Zaidi ya uchunguzi wa kimatibabu, kutakuwa na fomu ya uchunguzi wa afya ya jumla ya mtoto itakayojazwa kwa ajili ya mtoto wako ya kutumwa kwa shule yake, na atapokea chanjo zake zote ili aweze kuandikishwa shuleni haraka iwezekanavyo. Fomu hizi za shule zitapatikana tu utakapomaliza kufanyiwa uchunguzi kamili, ambao unaweza kuchukua kati ya ziara 1 hadi 3.

4. Kwa nini unahitajika kufanyiwa uchunguzi wa afya?

- Ili kuhakikisha wewe, familia yako na jamii yako mko salama na wenye afya.
- Ili kupata matibabu na dawa zinazohitajika.
- Ili kukupa hati muhimu za matibabu.

5. Je, unajiandaaje kwa uchunguzi wa afya?

- Beba hati zinazopatikana za kila mwanafamilia, kama vile: Fomu za I94, pasipoti, rekodi za matibabu, maelezo ya chanjo kutoka nyumbani na hati nyingine za utambulisho unazoweza kuwa nazo.
- Pakia vyakula vyepesi, maji, nepi za ziada au kitu kingine chochote unachoweza kuhitaji wakati unasubiri. Miadi inaweza kuchukua saa kadhaa, kwa sababu madaktari watajaribu kuchunguza wanafamilia wako wote kwa siku moja ili kupunguza idadi ya mara unazopaswa kwenda katika vituo vyao.
- Fika kwa wakati ili uepuke kucheleweshwa zaidi au kughairiwa kwa miadi yako. Nyakati za kuhudhuria miadi huzingatiwa sana nchini Marekani.
- Ikiwa hali ya dharura au hitaji la dharura litatokea, tafadhali mjulishe mtoa huduma wako wa jamii haraka iwezekanavyo ikiwa huwezi kuhudhuria miadi yako.

6. Je, unapaswa kutarajia nini katika uchunguzi wa afya?

- Kwanza, *utaandikishwa na mhudumu wa dawati la kujiandikisha*.
- Kisha, *utasubiri kwenye chumba cha kusubiri* ili uitwe na daktari. Tafadhali usiondoke isipokuwa kwa dharura. Ikiwa unahitaji kutumia chumba cha kujisaidia, usisite kuuliza mahali kilipo. Julisha mhudumu wa dawati la kujiandikisha ikiwa ni lazima utoke nje.
- Ikifika zamu yako, *utaelekezwa kwenye chumba cha faragha cha uchunguzi* ambapo daktari atawachunguza wanafamilia wote.
- Wakati wa uchunguzi, mhudumu wa afya atakufanyia uchunguzi wa mwili na kukuuliza baadhi ya maswali kuhusu afya yako ya mwili na kihisia.
- Mhudumu wa afya atahitaji kujua *jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, na anwani* ya kila mwanafamilia. Tafadhali hakikisha umeandika maelezo haya kwenye karatasi.
- *Tafadhali kumbuka kwamba shughuli zote za uchunguzi zinahitaji uchunguzi wa damu*. Uchunguzi huu utafanyiwa katika kliniki au utafanyiwa mahali pengine.
- Shughuli nyingi za uchunguzi zinahitaji pia sampuli ya kinyesi. Unaweza kupewa vifaa vya kwenda navyo nyumbani na maelekezo ya jinsi ya kukusanya sampuli ya kinyesi chako na kuja nayo kwenye kliniki wakati wa miadi yako ya ufuatiliaji.
- Tafadhali hakikisha umefanyiwa uchunguzi huu wote na umehudhuria miadi yoyote ya baadaye ya ufuatiliaji kwa wakati unaofaa. Uchunguzi wako kamili wa afya kwa kawaida hukamilika ndani ya ziara mbili au tatu, kwa hivyo miadi yako inayofuata ni muhimu.
- Baada ya kukamilishwa kwa uchunguzi wako, unaweza *kuomba nakala iliyochapishwa* ya fomu yako ya uchunguzi wa kimatibabu kwa ajili ya rekodi zako. Utapokea hati nyingine yoyote muhimu baada ya ziara zako za ufuatiliaji na kukamilika kwa uchunguzi, ikijumuisha hati muhimu za matibabu za watoto wako ili kuandikishwa shuleni.

7. Haki zako ni zipi wakati wa uchunguzi wa afya?

- Kila mwanafamilia ana haki ya kupata *matibabu na huduma sawa za kitaalamu*.
- Una haki ya kupata *huduma za ukalimani bila malipo*. Hizi kwa kawaida hutolewa kwa njia ya simu.
- Una *haki ya kukataa huduma zozote* wakati wa uchunguzi. Huduma ya uchunguzi wa kimatibabu imeundwa kwa kuzingatia afya na ustawi wako, lakini kama mgonjwa una haki ya kuidhinisha au kukataa huduma zozote za matibabu.
- Una haki ya *kueleza haja yako ya kuchunguzwa na daktari wa jinsia maalum*. Uliza mtoa huduma wako wa jamii kabla ya kuhudhuria miadi. Anaweza kuwasiliana na kliniki ili kujaribu kuweka mpango huu.
- Una haki ya *kuambatana na mtu mwingine* kwenye chumba cha uchunguzi, kwa kuzingatia kanuni za kliniki kuhusu kuambatana na watu wengine. Wazazi wanaweza kuambatana na watoto wao kila wakati.
- Una haki ya *faragha*, chini ya sheria ya Marekani inayojulikana kama HIPAA. Maelezo yako yote ya binafsi na ya afya yatawekwa kwa siri.